33. Makadirio.
34. Hesabu.
35. Ukaguzi.
36. Taarifa ya Mwaka ya utekelezaji.

**SEHEMU YA TANO  
MAKOSA NA ADHABU**

37. Makosa na adhabu.


SEHEMU YA SITA  
MASHARTI MENGINEYO

38. Kanuni.
39. Kufutwa na masharti yanayoendelea.
40. Ukinzani na sheria nyingine.



**Na.9**      *Muswada wa Sheria ya Takwimu*      **2015**      **5**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



NA.9 YA 2015

NAKUBALI,

JAKAYA MRISHO KIKWETE

*Rais*

11 Mei, 2015

**Sheria inayofuta Sheria ya Takwimu, kuanzisha Ofisi ya Taifa ya Takwimu, na Bodi ya Usimamizi wa Takwimu, kuweka masharti yanayohusu uratibu wa Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu, na kuweka masharti bora kuhusiana na majukumu ya Ofisi na Bodi, na masharti mengine yanayohusiana na hayo.**

[.....]

**IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

**SEHEMU YA KWANZA  
MASHARTI YA UTANGULIZI**

Jina la Sheria na tarehe ya kuanza kutumika

**1.** Sheria hii itaitwa Sheria ya Takwimu, ya mwaka 2015 na itanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri anaweza, kwa tangazo itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, kuiteua.

Matumizi

**2.** Sheria hii itatumika Tanzania Bara kuhusu masuala yote yaliyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu na itatumika Tanzania Zanzibar kuhusiana na masuala ya Sensa ya Watu na Makazi.

Tafsiri

**3.** Katika Sheria hii isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

“wakala au mawakala” inajumuisha taasisi za utafiti, mashirika yasiyo ya kiserikali, washirika wa maendeleo au mtumiaji mwingine au wazalishaji wengine wowote wa takwimu;

“afisa muidhiniwa” maana yake ni mtu aliyeteuliwa kwa maana hiyo chini ya kifungu cha 15;

“Bodi” maana yake ni Bodi ya Taifa ya Takwimu iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 7;

“ofisi” maana yake ni Ofisi ya Taifa ya Takwimu kama ilivyoelezewa kwenye Sheria hii;

“Sensa” maana yake ni shughuli ya uchukuaji wa taarifa za watu au vitu vyote vinavyokusudiwa katika maeneo yote husika;

“Mkurugenzi Mkuu” maana yake ni Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Takwimu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 9;

“taasisi za Serikali” inajumuisha Wizara, idara za Serikali Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

“Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya takwimu;

“Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu” maana yake ni mfumo unaoratibiwa na Ofisi ambao unajumuisha watoa taarifa, wazalishaji au watumiaji wa takwimu, na taasisi za utafiti na mafunzo;

“mtumishi” maana yake ni mtumishi yeyote aliyeajiriwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu;

- “takwimu rasmi” maana yake ni takwimu zinazotambuliwa na kutambulika kuwa rasmi chini ya kifungu cha 20;
- “sensa ya watu na makazi” maana yake ni sensa inayoendeshwa na Ofisi ya Takwimu chini ya kifungu cha 9;
- “mlalamikiwa” maana yake ni mtu yeyote anayetoa au kutakiwa kutoa taarifa za kitakwimu;
- “marejesho” maana yake ni kitabu chochote, nyaraka, fomu, kadi, kinasa sauti, santuri au kitu chochote ambacho kinahifadhi taarifa inayotakiwa kuingizwa au kurekodiwa au inatakiwa kuingizwa au kurekodiwa kwa madhumuni ya kitakwimu chini ya Sheria hii;
- “uchukuaji wa sampuli” maana yake ni utaratibu wa kitakwimu ambao vyao taarifa kuhusiana na eneo zima la utafiti zinapatikana kwa kutumia mbinu za kitakwimu zinazohusu taarifa zilizopatikana kuhusu uwiano wa idadi nzima ya watu au shughuli inayohusu eneo zima la utafiti;
- “takwimu” maana yake ni taarifa zinazohitajika kwa ajili ya kukusanya taarifa za kitakwimu, zinazopatikana kutokana na sensa na utafiti wa kitakwimu au kumbukumbu za kiutawala;
- “mtafiti/mtakwimu” maana yake ni mtu aliye na sifa za kielimu na stahhada ya takwimu;
- “kitengo cha takwimu” maana yake ni kitengo, divisheni au idara iliyoanzishwa katika taasisi yoyote ya Serikali kwa madhumuni ya kutekeleza makujumu yake ya kitakwimu;
- “utafiti” inajumuisha utafiti wa shughuli au watu ambapo taarifa inakusanywa kutoka kwenye sampuli yake kwa ujumla au kwa sehemu kwa madhumuni ya kitakwimu;

“shughuli” maana yake ni shughuli yoyote ya kitakwimu inayofanywa kwa njia ya biashara iwapo biashara hiyo inaendeshwa kwa madhumuni ya kuingiza faida au la na inajumuisha Wizara au Idara ya Serikali, chombo kilichopo kisheria, mamlaka ya serikali za mitaa au aina nyingine ya jumuiya au kundi la watu au sehemu yake yoyote ile.

## SEHEMU YA PILI

## OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU NA BODI YA USIMAMIZI

*(a) Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

Muendelezo wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**4.-**(1) Itaendelea kuwepo Ofisi ya Taifa ya Takwimu ambayo itajulikana kwa jina lake la ufupisho kama “NBS”.

(2) Ofisi itakuwa ni taasisi huru ya umma chini ya Wizara iliyo na dhamana na masuala ya Takwimu.

Hadhi ya Ofisi

**5.** Ili kulinda na kuendeleza uadilifu katika kushughulikia takwimu rasmi, Ofisi itakuwa na uhuru wa kitaaluma kuhusiana na namna ya ukusanyaji, uchambuzi, kutathmini na kusambaza taarifa za kitakwimu.

Majukumu ya Ofisi ya Takwimu

**6.-**(1) Ofisi ya Takwimu itakuwa ni Ofisi ya Taifa ya Takwimu itakayo wajibika kwa uzalishaji, uratibu, usimamizi na usambazaji wa takwimu rasmi nchini.

(2) Bila kuathiri ujumla wa masharti ya kifungu kidogo cha (1), Ofisi -

(a) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali wa Zanzibar itaendesha sensa ya watu na makazi;



- (b) itaishauri Serikali na umma kwa jumla, kuhusu masuala yote ya takwimu rasmi;
  - (c) itatoa taarifa za kitakwimu kwa umma zenye ubora wa hali ya juu, za uhakika na kwa wakati;
  - (d) itaandaa na kutunza sehemu moja ya utunzaji wa taarifa rasmi za kitakwimu, machapisho, nyaraka na taarifa zote za ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano;
  - (e) itaandaa mbinu, viwango, maneno na tafsiri kwa ajili ya kutengeneza takwimu rasmi;
  - (f) itasimamia taarifa rasmi za kitakwimu; na
  - (g) itaratibu na kusimamia Mfumo wa Taifa wa Takwimu Nchini;
  - (h) itatekeleza majukumu yote muhimu au yanayohitajika kwa madhumuni ya Ofisi chini ya Sheria hii.
- (3) Ofisi, Katika kutekeleza majukumu yake, inaweza kuingia kwenye mkataba na taasisi au watu binafsi kwa yeyo vigezo na masharti kwa kadri iatakvyo kubalika na wahusika wa mkataba.
- (4) Ofisi, kuhusiana na majukumu yanaohusiana na Tanzania Zanzibar, itatekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

*(b) Chombo cha Usimamizi*

Uanzishwaji na Muundo wa Bodi

7.-(1) Kinaanzishwa chombo cha usimamizi wa Ofisi itakayojulikana kama ya Bodi ya Ofisi ya Takwimu ya Taifa.

(2) Bodi itaundwa na-

- (a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye ujuzi na uzoefu katika masuala ya takwimu, hisabati, uchumi au uelewa katika masuala ya usimamizi wa biashara; na

(b) wajumbe wa nane, wenye vyeo vya Afisa Mkuu watakaoteliwa na Waziri baada ya kuteuliwa na taasisi zao husika kama ifuatavyo:

- (i) mwakilishi wa Benki kuu ya Tanzania;
- (ii) mwakilishi kutoka katika Wizara yenye dhamana ya masuala ya takwimu;
- (iii) mwakilishi kutoka katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- (iv) mwakilishi kutoka katika Ofisi ya Waziri Mkuu;
- (v) mwakilishi kutoka katika Tume ya Mipango;
- (vi) Mwenyekiti wa Bodi ya Takwimu ya Zanzibar;
- (vii) mwakilishi kutoka katika Taasisi za Elimu ya Juu;
- (viii) mjumbe mmoja atakayeteuliwa kutoka miongoni mwa watumiaji au wazalishaji wa takwimu kutoka katika sekta binafsi.

Majukumu ya bodi

8. Majukumu ya Bodi yatajumuisha-

- (a) kuidhinisha na kufuatilia utekelezaji wa sera kuhusiana na Ofisi;
- (b) kuidhinisha muundo, mipango ya uendelezaji wa taaluma, ngazi za ajira za watumishi na vigezo na masharti kuhusiana na utumishi wa watumishi wa Ofisi;

- (c) kuhidhinisha uteuzi wa watumishi wa ngazi za utawala;
- (d) kuidhinisha hatua za kinidhamu zitakazochukuliwa dhidi ya watumishi wa wa ngazi za utawala katika Ofisi;
- (e) kuidhinisha mpango wa shughuli za Ofisi ofisi, mpango-kazi wa mwaka na bajeti ya mwaka;
- (f) kumfahamisha Waziri maendeleo ya shughuli za Ofisi kila baada robo ya mwaka; na
- (g) kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa kadri itakavyoelekezwa na Waziri kwa maandishi.

Uteuzi wa  
Mkurugenzi  
Mkuu

**9.**-(1) Rais atamteua Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Takwimu kufuatia mapendekezo ya Waziri.

(2) Mtu hatakuwa na sifa za kupendekezwa na kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu isipokuwa kama ana na shahada au elimu nyingine ya juu tasnia ya takwimu au Uchumi au Hisabati na awe angalau na uzoefu wa anagalau miaka mitano katika tasnia ya takwimu na pia awe na uwezo wa uongozi uliothibitika.

(3) Mkurugenzi Mkuu atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitano na kwa kiwango cha kuridhisha cha utendaji kazi wake, anaweza kuteuliwa tena.

Kutenguliwa  
kwa uteuzi

**10.** Rais anaweza, kufuatia mapendekezo ya Waziri, kusitisha uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu kutokana na-

- (a) utovu wa nidhamu;
- (b) kushindwa au kutokuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu ya ofisi yake kutokana na udhaifu wa mwili au akili; au

(c) kutokuwa na uwezo kiutendaji.

**Majukumu**  
ya  
Mkurugenzi  
Mkuu

**11.** Mkurugenzi Mkuu atakuwa Mtendaji Mkuu wa Ofisi na atawajibika kwa shughuli za kila siku za Ofisi, ikijumuisha kusimamia fedha, mali na shughuli za Ofisi na usimamizi wa maofisa na watumishi wa Ofisi.

Kaimu  
Mkurugenzi  
Mkuu

**12.**-(1) Endapo nafasi ya Mkurugenzi Mkuu inakuwa wazi au iwapo Mkurugenzi Mkuu anashindwa kutekeleza majukumu ya ofisi yake, Waziri atamteua mtu mwingine mwenye ujuzi stahiki au uzoefu, kuwa kaimu Mkurugenzi Mkuu kwa kipindi ambacho nafasi hiyo itakuwa wazi au kwa kipindi ambacho Mkurugenzi Mkuu ameshindwa kutekeleza majukumu yake.

(2) Mtu anayekaimu kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) hatakaimu kwa kipindi kinachozidi miezi sita:

Isipokuwa kwamba, Waziri anaweza kwa sababu za msingi, kuongeza kipindi cha kukaimu kisichozidi miezi sita.

(3) Masharti ya kifungu kidogo (2) hayatatumika iwapo Mkurugenzi Mkuu atakuwa nje ya ofisini kwa muda mfupi kutokana na sababu ya utekelezaji wa majukumu ya kiofisi, ambapo katika hali hiyo, Mkurugenzi Mkuu atakasimisha majukumu ya ofisi yake kwa mmoja wa watumishi walio katika ngazi ya utawala.

Wafanyakazi  
wengine

**13.** Kwa kuzingatia sheria kuhusiana na masuala ya ajira, Mkurugenzi Mkuu atasababisha kuajiriwa kwa idadi ya watumishi kwa kadri atakavy atakapona inafaa au inahitajika kwa ajili ya utekelezaji wenye tija wa mamlaka na majukumu ya ofisi.

**Na.9** *Muswada wa Sheria ya Takwimu* **2015** 13

Kiapo cha  
kutunza  
siri/**kiapo cha**  
**usiri**

**14.**-(1) Mtu yeyote, mbali na mtumishi wa Ofisi aliyeajiriwa kutekeleza jukumu lolote linalohusu uzalishaji wa takwimu chini ya Sheria hii, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yake, atakula kiapo cha kutunza siri au atathibitisha kuwa atakutunza siri mbele ya Kamishna wa viapo kwa namna iliyoainishwa kwenye Jedwali la Pili.

(2) Kwa madhumuni ya Kifungu kidogo cha (1), mtu aliyeajiriwa kama karani kwenye sensa ya watu na makazi, atatoa tamko la maandishi kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na kuliwasilisha tamko hilo kwa Afisa aliyeidhinishwa au mtumishi wa Ofisi kwa namna iliyoainishwa kwenye Jedwali la Pili.

Maofisa  
walioidhinishwa/w  
**aidhinishwa**

**15.** Mkurugenzi Mkuu anaweza kuteua watumishi wa Ofisi kuwa maafisa walioidhinishwa/waidhinishwa kwa masharti ya muda na vigezo, kwa madhumuni ya kutekeleza shughuli za kitakwimu chini ya Sheria hii, kwa kadri atakavyoamua.

**Kinga dhidi ya**  
**uwajibikaji**

**16.** Hakuna kitendo kiichofanywa na afisa au mwajiriwa wa Ofisi, iwapo kimefanywa kwa nia njema katika utekelezaji au katika utekelezaji unaodhaniwa kuwa umetekelezwa au katika utekelezaji wa wajibu wake au majukumu yake kama afisa au mwajiriwa wa Ofisi kitakacho mwajibisha mwajiriwa huyo au afisa, kufanya kitendo chochote, kuwajibika au kushitakiwa kwa njia yoyote ile.

Mfumo wa Kitaifa  
wa Takwimu na  
uratibu wake

**17.**-(1) Kutakuwa na Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu utakaojulikana kwa jina lake la ufupisho “NSS” ambao utasimamiwa na **Ofisi**.

(2) Kwa kuzingatia kifungu cha 6, Ofisi itaratibu Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu kwa lengo la kuwa na mfumo wa mmoja wakitakwimu ili kuhakikisha utumiaji unaofaa wa rasilimali zilizopo.

(3) Katika utekelezaji jukumu yake ya kiuratibu chini ya kifungu hiki, Ofisi ita-

- (a) toa kanuni za utendaji kwa jili ya takwimu rasmi ambazo zitaonesha viwango vya weledi wa kufuatwa na wakala wote wa uzalishaji wa takwimu rasmi;
- (b) anzisha na kuendeleza kikamilifu benki ya data ya kitaifa kwa kutumia benki za data za kisekta zilizoanzishwa na wakala mbalimbali;
- (c) weka viwango kwa ajili ya ukusanyaji, uchambuzi na uchapishaji wa takwimu ili kuhakikisha ulinganifu wa ujumla na usahihi wa taarifa za kitakwimu;
- (d) toa mwongozo na msaada mwingine kwa kadri itakavyohitajika na watumiaji au watoa takwimu; na
- (e) kuza ushirikiano na usawa kati ya watumiaji au watoaji wa takwimu kwa lengo la kudurufu jitihada na kuhakikisha matumizi kamili ya rasilimali chache zilizopo.

Uhusiano na wakala nyingine

**18.-(1)** Kwa kuzingatia sheria hii na bila kuathiri masharti ya kifungu cha 20, Mkurugenzi Mkuu pekee ndiye anayeweza kuanzisha/kuidhinisha ukusanyaji wa takwimu rasmi au kubadilisha au kusitisha zoezi la ukusanyaji wa takwimu rasmi.

(2) Bila kujali ya sheria nyingine yoyote, hakuna mtu au wakala atakaye idhinisha kuanza kwa zoezi la ukusanyaji wa takwimu rasmi isipokuwa kwa ridhaa ya Mkurugenzi Mkuu.

Ugatuaji wa madaraka ya ukusanyaji wa takwimu

**19.** Bila ya kujali ujumla wa masharti yaliyomo katika kifungu kidogo cha 18(2), Mkurugenzi Mkuu itachukuliwa kuwa amekasimu mamlaka yake kwa wakuu wa wakala ambao sheria zao zinawapa mamlaka ya kukusanya taarifa za kitakwimu kuhusiana na maeneo yao ya utendaji.

Takwimu rasmi

**20.**-(1) Takwimu Rasmi zitakuwa ni takwimu zinazotengenezwa na:

- (a) Ofisi;
- (b) taasisi za Serikali; na
- (c) wakala.

(2) Takwimu zinazozalishwa chini ya kifungu kidogo cha 1(c) zitakuwa na sifa za kuwa takwimu rasmi iwapo zinakidhi vigezo na viwango vilivyowekwa na Ofisi, na zimeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu.

(3) Kwa madhumuni ya uhuwishaji, Ofisi inaweza kuweka mbinu na viwango vya kitakwimu ili kusaidia ukusanywaji na ulinganishaji wa takwimu rasmi zilizotolewa kitaifa na kimataifa.

SEHEMU YA TATU  
UKUSANYAJI NA USAMBAZAJI WA TAARIFA

Sensa ya watu na makazi **muongo mmoja**

**21.**-(1) Rais anaweza, kwa Amri itakayochapishwa katika *Gazeti la Serikali* kuagiza kufanyika kwa Sensa ya Watu na Makazi katika Jamhuri ya Muungano au sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano kama itakavyoainishwa na Amri hiyo.

(2) Amri iliyotolewa chini kifungu kidogo (1), inaweza kutaja tarehe ambayo au kipindi ambacho sensa hiyo itafanyika, taarifa zitakazokusanywa katika Sensa na kipindi ambacho sensa hiyo itafanyika.

Ukusanyaji wa takwimu nyingine

**22.**-(1) Ofisi inaweza kukusanya takwimu kuhisiana na mambo yote au yoyote kati ya mambo yaliyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria hii.

(2) Ofisi inaweza kusababisha takwimu zilizokusanywa, na taarifa yoyote rasmi za kitakwimu, iliyowekwa wazi kuchapishwa.

Ukusanyaji wa pamoja

**23.**-(1) Ofisi inaweza kuingia katika makubaliano na wakala yoyote juu ya ukusanyaji wa pamoja wa taarifa za kitakwimu kwa kadiri itakavyohitajika.

(2) Mfanyakazi wa wakala yeyote, iwapo atahusishwa kwenye zoezi la ukusanyaji wa taarifa kwa pamoja au uchambuzi wa taarifa zilizokusanywa ktika zoezi la ukusanyaji wa pamoja, atatoa tamko la kutunza siri ambalo ni sawa na tamko la kutunza siri lililoainishwa kwenye kifungu cha 14, bila kujali tamko la kutunza siri lililotolewa chini ya Sheria nyingine yeyote.



**Uchukuaji  
Sampuli**

**24.**-(1) Takwimu kuhusiana na mambo yote au baadhi ya mambo yaliyoainishwa katika Jedwali la Tatu, zinaweza kukusanywa kwa njia ya sampuli katika mahali penye rekodi zilizokamilika, pale ambapo matumizi ya utaratibu huo utaonekana kuwa haufai.

(2) Sampuli zilizokusanywa katika kifungu kidogo cha (1) zinaweza pia kutumika katika madodoso ya majaribio pamoja na mchakato wa kitakwimu kabla ya kukamilika.

(3) Haitakuwa kinga kwa mtu yeyote atakayeshindwa kujaza dodoso na kurudisha au kujibu maswali lolote kwa sababu sehemu tu au kundi fulani la watu linatakiwa kujaza dodoso au kujibu maswali hayo.

**Udhibiti wa utoaji  
wa taarifa**

**25.**-(1) Taarifa zifuatazo hazitachapishwa, kukubalika katika ushahidi au kuonyeshwa kwa mtu yeyote ambaye si mwajiriwa katika kutekeleza jukumu lililotolewa chini ya Sheria hii, isipokuwa tu kwa kibali cha awali cha maandishi kutolewa na mtu aliyetoa taarifa au kujibu swali hilo, au kama ni masuala ya kazi au shughuli, kutoka kwa mtu mwenye madaraka, usimamizi au uangalizi wa kazi au shughuli hiyo:

- (a) taarifa binafsi au sehemu ya taarifa hiyo;
  - (b) jibu lolote lililotolewa kwa swali lolote lililoulizwa kwa madhumuni ya Sheria hii;
  - (c) taarifa, sehemu ya taarifa au nyaraka nyingine yoyote iliyo na maelezo kuhusiana na taarifa hiyo au jibu litakalo wezesah utambuzi wa maelezo ya mtu yeyote, biashara au shughuli.
- (2) Kifungu kidogo cha (1) hakitatumika iwapo-

- (a) mtu, biashara au shughuli imechapisha marejesho, majibu, taarifa, wazo au nyaraka na kuweka data kwenye kompyuta kwa ajili ya matumizi ya umma; au
- (b) marejezo hayo, majibu au taarifa na nyaraka hizo zinahitajika kwa madhumuni ya kuendesha mashitaka.

Msamaha kwa  
utoaji wa taarifa

26. Bila kujali masharti ya kifungu cha 25, Ofisi inaweza kutoa:

- (a) taarifa za umma chini ya sheria yoyote au nyaraka ya umma;
- (b) taarifa iliyoko katika hali ya fahirisi au orodha ya majina na anuani za shughuli za mtu binafsi au biashara pamoja na namba za simu ambazo anaweza kupatikana maelezo ya kitasnia yaliyotolewa kwake, bidhaa anazozalisha, anazotengeneza, anazosafirisha, anazotunza, anazonunua, au anazouza au huduma anazotoa wakati wa utekelezaji wa shughuli zao na idadi ya watu waliohusishwa;
- (c) maelezo ya kina ya biashara ya nje, safari za meli na ndege na mizigo inayoshughulikiwa bandarini; au
- (d) taarifa kuhusiana na mamlaka za serikali za mitaa au chombo kingine kilichopo kisheria.

**Na.9** *Muswada wa Sheria ya Takwimu* **2015** **19**

Uwekaji wazi wa taarifa zisizotambuliwa

**27.**-(1) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2) Ofisi inaweza kuweka wazi taarifa zilizo kwenye kumbukumbu za kitakwimu za mtu binafsi kwa madhumuni pekee ya utafiti au ya kitakwimu, isipokuwa kwamba:

(a) taarifa zote za utambulisho kama vile jina na anuani ya mlalamikiwa zimeondolewa;

(b) taarifa zinatolewa kwa namna ambayo si rahisi kuwezesha utambulisho wa mtu huyo au biashara inayohusika kufahamika.

(2) Kila mtu ambaye kwake taarifa za kitakwimu zimetolewa kwake kwa mujibu wa kifungu hiki -

(a) hatajaribu kumtambulisha mtu yeyote au au biashara;

(b) atatumia taarifa kwa ajili ya utafiti na madhumuni ya kitakwimu tu;

(c) hatatoa taarifa hizo kwa mtu mwingine au asasi;

(d) atatekeleza maelekezo yoyote yaliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu kuhusiana na kumbukumbu hizo.

Usalama wa taarifa zilizorekodiwa

**28.** Ofisi itachukua hatua zote muhimu kuhakikisha usalama na usiri wa taarifa za kitakwimu zilizokusanywa au kutolewa na ofisini na mawakala wengine zinawekwa kwa mujibu wa sheria hii.

Kuharibiwa kwa fomu na marejesho ya mtu binafsi

**29.**-(1) Ofisi au kila wakala, watatoa taarifa kuharibu sensa zote za mtu binafsi na fomu za tafiti na marejesho zilizotumika kwa madhumuni ya Sheria hii baada ya taarifa hizo kufanyiwa kazi, kuhalalishwa na kutangazwa.

(2) Fomu za sensa za mtu binafsi na fomu za utafiti zilizo rejewa chini ya kifungu kidogo cha (1) zitaharibiwa ndani ya kipindi cha miaka mitano tangu taarifa hizo zilipotumika, kuhakikiwa na kuchapishwa.

Mamlaka ya kupata maelezo

**30.**-(1) Endapo sense yoyote au utafiti unafanywa au takwimu nyingine zinakusanywa kwa mujibu wa Sheria hii, afisa aliyeidhinishwa/ muidhinishwa au mtumishi wa Ofisi anaweza, kwa namna iliyoelezewa katika kifungu kidogo cha (2), kumtaka mtu yeyote kumpatia maelezo kama ilivyo ainishwa au maelezo kwa kadri ambavyo Mkurugenzi Mkuu atakavyoona inafaa kuhusiana na kufanyika kwa sensa au ukusanyaji wa takwimu hizo.

(2) Mtu atakaye takiwa kutoa maelezo kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), kwa kadiri ya uelewa wake, taarifa na uamini wake, ata jaza fomu, kufanya marejesho hayo, kujibu maswali hayo na kutoa taarifa zote kwa namna na ndani ya muda kama utakao ainishwa na afisa aliyeidhinishwa/muidhinishwa au mtumishi wa Ofisi.

(3) Afisa aliyeidhinishwa au mtumishi wa Ofisi wanaweza, katika muda wowote wa kawaida na baada ya kuonesha kuidhinishwa kwake anaweza-

(a) kuhusiana na sensa au tafiti, kuingia na kukagua jengo lolote ikijumuisha nyumba; na

- (b) kuhusiana na ukusanyaji wa takwimu nyingine, na kukagua jengo lolote ambamo shughuli zinazotoa faida zinaendeshwa, na katika hali nyingine nyingine anaweza kuhoji kwa kadri itakavyoonekana kuwa ni muhimu kwa ajili ya ukusanyaji wa sense au takwimu, kama itakavyo kuwa.

Upatikanaji wa kumbukumbu

**31.**-(1) Endapo Mkurugenzi Mkuu anaona kuwa ukusanyaji wa takwimu kuhusiana na jambo lolote zinaweza kupatikana kutoka kwenye taasisi yoyote ya Serikali, wakala au mtumiaji au mzalishaji wa takwimu, atatoa idhini kwa afisa aliyeidhinishwa au mtumishi wa Ofisi kwa madhumuni ya kupata taarifa inayohitajika.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), taarifa zilizopatikana zitahusu masuala ya ukusanyaji wa takwimu ambayo yameidhinishwa au kuelekezwa au kwa ajili ya ukamilishaji au ukusanyaji wa takwimu.

SEHEMU YA NNE  
MASHARTI KUHUSIANA NA FEDHA

Vyanzo vya mapato vya Ofisi

- 32.** Fedha na raslimali za Ofisi zitatokana na-
- (a) fedha inayotengwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi;
  - (b) fedha zilizopelekewa kutokana na bidhaa na huduma zinazotolewa na Ofisi;
  - (c) kiasi cha fedha kilichokopwa, kilichopokelewa na au kilichotolewa kwa Ofisi kwa madhumuni ya utekelezaji wa majukumu yake; na

- (d) michango, misaada na zawadi kwa kadri ambavyo Ofisi itapokea kutoka kwa mtu au kundi la watu.

Makadirio

**33.**-(1) Mkurugenzi Mkuu, si zaidi miezi mitatu kabla ya kwisha kwa kila mwaka wa fedha, atandaa na kuwasilisha kwenye Bodi mpango kazi na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Bodi itawasilisha kwa Waziri, mpango kazi na makadirio yaliyoandaliwa chini ya kifungu kidogo cha (1), kwa ajili ya idhini yake.

(3) Hakuna matumizi yatakayofanywa kwa kutumia fedha za Ofisi isipokuwa kama matumizi hayo ni sehemu ya madirio ya matumizi yaliyoidhinishwa na Waziri chini ya kifungu kidogo cha (2).

Hesabu

**34.**-(1) Ofisi itatunza kumbukumbu sahihi ya vitabu vya hesabu.

(2) Kwa kuzingatia maelekezo yoyote yaliyotolewa na Bodi, Mkurugenzi Mkuu ataandaa maelezo kuhusiana na kila mwaka wa fedha, na na si zaidi ya miezi mitatu baada ya kufungwa kwa mwaka wa fedha, taarifa ambayo itajumuisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi kwa kipindi hicho cha mwaka.

(3) Taarifa iliyoandaliwa chini ya kifungu kidogo cha (2) zitakuwa na-

- (a) mizania na taarifa ya mapato na matumizi ya Ofisi kwa ajili ya mwaka huo wa fedha; na
- (b) taarifa nyingine kuhusiana na masuala ya kifedha ya kwa kadri ambavyo Waziri anaweza kuhitaji kwa maandishi.

Ukaguzi

**35.**-(1) Hesabu za Ofisi kuhusiana na kila mwaka wa fedha zitakaguliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali au Mkaguzi atakaeteuliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(2) Mkurugenzi Mkuu, ndani ya miezi mitatu baada ya kufunga mahesabu ya mwaka wa fedha, atawasilisha kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali taarifa ya hesabu kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 34 cha Sheria hii, kwa ajili ya ukaguzi.

(3) Mkurugenzi Mkuu mapema iwezekanavyo, isipokuwa si zaidi ya miezi miwili baada ya kupokea taarifa ya ukaguzi kutoka kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, atawasilisha kwa Waziri maelezo ya taarifa ya fedha yaliyokaguliwa pamoja na taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kuhusiana na maelezo hayo.

Taarifa ya Mwaka  
ya Utekelezaji

**36.** Bodi itandaa na kuwasilisha kwa Waziri ndani ya miezi mitatu baada ya kufungwa kwa kila mwaka wa fedha, taarifa ya mwaka juu ya utendaji wa Ofisi kwa mwaka huo wa fedha na Waziri atasababisha nakala ya taarifa hiyo kuwasilishwa Bungeni.

#### SEHEMU YA TANO MAKOSA NA ADHABU

Makosa na  
Adhabu

**37.**-(1) Mtu yeyote ambaye-

- (a) kwa mujibu wa nafasi ya kazi yake anapata taarifa yeyote inayoweza kuathiri thamani ya soko la hisa yoyote au amana zingine, riba, bidhaa au kitu na ambaye kabla ya taarifa hizo hazijatolewa kwa umma, atatumia moja kwa moja taarifa hizo au kwa kificho kwa manufaa binafsi;

- (b) bila ya mamlaka halali, anachapisha au kutoa kwa mtu mwingine yeyote vinginevyo, mbali na kwa mujibu wa utendaji kazi wake, taarifa ambayo ameipata kwa mujibu wa nafasi yake;
- (c) anatelekeza jukumu lake au kwa makusudi anatoa tamko lolote, kauli au marejesho katika utekelezaji wa kazi yake au anaelekeza kwa ajili ya kutoa taarifa zozote za kitakwimu za uongo;
- (d) katika utekelezaji wa majukumu yake, anajipatia au anajaribu kujipatia taarifa ambazo hajaidhinishwa kuzipata;
- (e) anaitisha, anapokea au anachukua, kuhusiana na ajira yak echini ya Sheria, kutoka kwa mtu yeyote, mbali na afisa wa umma aliyeidhinishwa ipasavyo, malipo ya aina yoyote au zawadi,
- anatenda kosa iwapo atatiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua milioni mbili au kutumikia kwa kipindi kisichopungua miezi sita, au vyote kwa pamoja.
- (2) Mtu yeyote ambaye anamiliki taarifa yoyote ya kitakwimu, ambazo kwa ufahamu wake anajua kuwa zimetolewa kinyume na masharti ya Sheria hii, anachapisha au anasambaza kwa watu wengine taarifa hizo, anatenda kosa, na iwapo atatiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano au kutumikia kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na mbili, au vyote kwa pamoja.
- (3) Mtu yeyote ambaye-



- (a) anamzuia afisa yeyote aliyeidhinishwa au mtumishi wa Ofisi katika utekelezaji halali wa yeyote kati ya majukumu yake au katika utekelezaji wa mamlaka yaliyotolewa kwake chini ya Sheria hii;
- (b) Anakataa au kwa makusudi anaacha:
- (i) kukamilisha na kusambaza ndani ya muda uliopangwa taarifa zinazotakiwa katika marejesho, fomu au nyaraka yoyote iliyoachiwa au iliyotumwa kwake; au
  - (ii) kujibu swali lolote lililoelekezwa kwake chini Sheria hii;
- (c) anatoa katika marejesho, fomu au nyaraka yeyote aliyojaza kwa mujibu wa Sheria hii, maelezo yoyote ya uongo;
- (d) bila mamlaka halali, anaharibu, anachafua au anachana marejesho, fomu au nyaraka yoyote iliyo na taarifa zilizokusanywa chini ya Sheria hii;
- (e) akijua si afisa aliyeidhinishwa au mfanyakazi wa Ofisi, anajipa sifa au kujitambulisha kuwa ni mfanyakazi wa Ofisi-
- (f) anamhamasisha au anamshauri mtu mwingine yeyote kushiriki kwenye shughuli kuhusiana na ukusanyaji wa taarifa chini ya Sheria hii;
- (g) anafanya kitu chochote ambacho hana haki ya kukifanya chini ya Sheria hii;

(h) pasipo kuwa na sababu za msingi, anakataa kutoa kumbukumbu au nyaraka kwa mujibu wa vifungu vya 30 na 31;

(i) anakiuka masharti ya Sheria hii ambayo kuhusiana nayo hakuna kosa mahususi lililotajwa,

anatenda kosa atawajibika, iwapo atatiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

(4) Mkurugenzi Mkuu, mdhibiti au mtu mwingine yeyote anayehusika na masuala ya usimamizi wa chombo chochote cha mawasiliano ambaye anasababisha kuchapishwa kwa taarifa rasmi za kitakwimu za uongo au anatangaza program yoyote kuhusiana na shughuli ya ukusanyaji wa data ambayo imefanywa au inafanywa na Ofisi ambayo inamsababisha mtu yeyote au watu kushindwa kushiriki kwenye zoezi la ukusanyaji wa data au kushirikiana na maafisa wa Ofisi, anatenda kosa atawajibika, iwapo atatiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

(5) Wakala au mtu anachapisha au anasambaza taarifa rasmi za kitakwimu ambazo zinaweza kupelekea upotoshwaji wa maelezo husika, anatenda kosa atawajibika, iwapo atatiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja.

(6) Mtu yeyote aliyeidhinishwa na Ofisi kushughulikia taarifa yoyote rasmi ya kitakwimu, kabla ya kuichapisha au kuitangaza taarifa hiyo kwa umma, atahakikisha kuwa anapata idhini ya Ofisi.

(7) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, “chombo cha mawasiliano” kinajumuisha kituo cha radio, kituo cha televisheni, gazeti au jarida, tovuti au chombo kingine chochote cha habari.

SEHEMU YA SITA  
MASHARTI MENGINEYO

Kanuni

**38.** Waziri anaweza, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii, kutunga Kanuni zitakazo-

- (a) kuelezea namna ambayo Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu utakavyoratibiwa;
- (b) ainisha kiwango cha ada na tozo vitakavyo lipwa kuhusiana na taarifa maalum au ripoti iliyotolewa au huduma maalumu za kitakwimu zilizotolewa ;
- (c) ongeza au kufuta, kutoa au vinginevyo kubadili mambo yaliyo ainishwa kwenye Jedwali la Tatu; na
- (d) kuhusiana na masuala yote ambayo kikawaida ni muhimu kwa mujibu wa sheria zinazo simamia masuala ya takwimu nchini kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.


Kufutwa na masharti yanayoendelea sura ya 351

- 39.**-(1) Sheria ya Takwimu imefutwa.
- (2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1)-
- (a) jambo lolote lililofanywa au hatua yoyote iliyochukuliwa kuwa limeganywa chini ya Sheria iliyofutwa, itachukuliwa kuwa imefanywa chini ya Sheria hii;
  - (b) uteuzi wowote uliofanywa chini ya Sheria iliyofutwa na ambao haujatenguliwa mara kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii utachukuliwa kuwa umefanywa chini ya Sheria hii na utaendelea kuwa na nguvu kisheria hadi pale utakapotenguliwa au uteuzi mpya utakapofanyika chini ya Sheria hii; na

(c) mwenendo wowote halali uliofanywa au Amri zilizotolewa chini ya Sheria iliyofutwa, zitaendelea na zitachukuliwa kuwa ni mwenendo au Amri vilivyotolewa chini ya masharti ya Sheria hii.

Ukinzani na sheria nyingine

**40.** Endapo masharti yoyote ya Sheria hii yanakinzana na masahiti ya Sheria nyingine yoyote kuhusiana na taarifa rasmi za takwimu, masharti ya Sheria hii yatakuwa na nguvu kwa kisai ambacho kulinzana huko kunahusika.



**JEDWALI LA KWANZA***(Limetengenezwa chini ya kifungu 7(5))*Muda wa  
uteuzi

**1.-(1)** Kila mjumbe wa Bodi ataendelea kuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe ya uteuzi wake na anaweza kuteuliwa tena.

(2) Bila kujali aya ndogo ya (1) ya aya hii, mjumbe anaweza kujiuzulu wakati wowote kwa kutoa notisi ya maandishi kwa mamlaka ya uteuzi na tangu tarehe hiyo iliyoainishwa kwenye notisi, au iwapo hakuna tarehe iliyotajwa kwenye notisi, kuanzia tarehe ambayo notisi ilipopelekwa na mamlaka ya uteuzi, mjumbe atakoma kuwa mjumbe.

(3) Mtu ambaye ni mjumbe kutokana na kushika madaraka katika ofisi nyingine yoyote atakoma kuwa mjumbe baada ya kuacha kushika madaraka katika ofisi ambayo kwa wadhifa huo amekuwa mjumbe.

Kufuta uteuzi

**2.** Pale ambapo mjumbe wa Bodi anashindwa kuhudhuria vikao vitatu vya Bodi mfululizo bila sababu za msingi, Bodi itaishauri mamlaka ya uteuzi kuhusu suala hili na mamlaka ya uteuzi inaweza kufuta uteuzi wa mjumbe huyo na kuteua mjumbe mpya badala yake.

Ukomo wa  
ujumbe

**3.** Iwapo mjumbe yeyote wa Bodi anakoma kuwa mjumbe kwa sababu ya kujiuzulu au kifo au kwa ya kushindwa kutekeleza majukumu yake kama mjumbe kwa sababu ya kutokuwepo ndani ya Jamhuri ya Muungano au kwa sababu ya udhaifu wa mwili au akili au iwapo mamlaka ya uteuzi inafuta uteuzi wake chini ya aya ya 2, mamlaka ya uteuzi inaweza kuteua mjumbe mwingine badala yake na mjumbe atakaye teuliwa kwa mujibu wa Jedwali hili atakuwepo madarakani kwa muda uliobakia wa mjumbe aliyemtangulia.

- Makamu Mwenyekiti
- 4.** Bodi itamchagua mmoja wa wajumbe wake kuwa Makamu-Mwenyekiti na mjumbe yeyote atakayechaguliwa kuwa Makamu-Mwenyekiti, na ataendelea kushika madaraka ya Makamu-Mwenyekiti kwa muda utakaopangwa na Bodi anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kuisha, kwa kuzingatia kigezo kuwa mjumbe huyo anaendelea kuwa mjumbe.
- Mamlaka ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti
- 5.**-(1) Mwenyekiti ataongoza mikutano yote ya Bodi.  
 (2) Iwapo katika mkutano wowote wa Bodi Mwenyekiti hata kuwepo, Makamu-Mwenyekiti ataongoza kikao hicho.  
 (3) Iwapo Mwenyekiti na Makamu-Mwenyekiti hawapo katika mkutano wowote wa Bodi, wajumbe waliopo, watumchagua Mwenyekiti wa muda kutoka miongoni mwao kuongoza kikao.  
 (4) Mwenyekiti, Makamu-Mwenyekiti au Mwenyekiti wa muda anayeongoza mkutano wowote wa Bodi, atakuwa na haki ya kupiga kura, na inapotokea mgongano wa kura, atakuwa na kura ya turufu mbali na kura yake ya kawaida.
- Mikutano na taratibu za Bodi
- 6.**-(1) Mkutano wa kawaida cha Bodi utaitishwa na Mwenyekiti na taarifa inayotaja sehemu, tarehe na muda wa kikao itatumwa kwa kila mjumbe mahala pake pa kawaida pa kazi au makazi kwa siku zisizopungua siku 14 kabla yatarehe ya kikao hicho.  
 (2) Bodi itafanya mkutano wa kawaida minne kwa mwaka, lakini Mwenyekiti anaweza akaitisha kikao cha dharura endapo hitaji la kufanya hivyo litajitokeza.  
 (3) Mwenyekiti wa Bodi anaweza kumwalika mtu yeyote ambaye si mjumbe kushiriki katika mjadala wa Bodi na mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.
- Akidi
- 7.** Mwenyekiti na wajumbe wengine watatu wataunda akidi ya Mkutano wa Bodi.

**Na. 9** *Muswada wa Sheria ya Takwimu* **2015** **31**

Uamuzi kwa njia ya maandishi	<p><b>8.-(1)</b> Bila kujali aya ya 7, Mwenyekiti anaweza kuelekeza uamuzi kufanywa na Bodi bila kufanya mkutano kwa kugawa nakala ya suala lililo mezani kwa wajumbe wote ili watoe maoni yao kwa maandishi.</p> <p>(2) Mjumbe yeyote atakuwa na haki ya kutaka uamuzi wowote kuahirishwa na uamuzi huo kujadiliwa kwenye mkutano wa Bodi.</p>
Muhtasari wa mkutano	<p><b>9.</b> Muhtasari wa kila kikao cha Bodi utatunzwa na utathibitishwa na Bodi katika kikao kinachofuata na kusainiwa na Mwenyekiti wa kikao hicho.</p>
Uhalali wa matumizi ya lakiri	<p><b>10.</b> Lakiri ya Bodi haitawekwa kwenye hati, nyaraka na miongozo mingine isipokuwa mbele ya Mwenyekiti na Mkurugenzi Mkuu, au Mwenyekiti au Mkurugenzi Mkuu na mjumbe mwingine mmoja ambaye atateuliwa na Bodi kwa ajili hiyo.</p>
Uthibitishaji wa nyaraka	<p><b>11.</b> Nyaraka zozote za Bodi, mbali na nyaraka nyingine zinazohitajika kisheria kuwekwa lakiri na maamuzi yote ya Bodi, vinaweza kuthibitishwa kwa kusainiwa na Mkurugenzi Mkuu au ofisa mwingine aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu kwa niaba yake.</p>
Uhalali wa vikao	<p><b>12.</b> Hakuna jambo au mwenendo wa Bodi utakao kuwa batili kwa sababu ya idadi ya wajumbe kutokamilika wakati wa kikao hicho kwa sababu ya idadi pungufu ya wajumbe wakati wa kufanya jambo hilo au mwenendo huo au kasoro zozote katika uteuzi wa mjumbe yeyote au kwamba mjumbe yeyote kwa wakati huo hakuwa na sifa au hastahili kuwa mjumbe.</p>
Bodi kusimamia shughuli zake	<p><b>13.</b> Kwa kuzingatia masharti ya Jedwali hili Bodi inaweza kujiwekea utaratibu wa kuendesha mwenendo wa shughuli zake.</p>

**JEDWALI LA PILI**

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 14(2) )*

Aidha;

Mimi.....naapa/nathibitisha kwamba nitatekeleza majukumu yangu kwa uaminifu na uadilifu kama.....kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Takwimu, na kwamba sitatoa taarifa yoyote ninayoipata kutokana na kazi yangu hii bila kibali halali.

**MTOA KIAPO**

Kiapo kimetolewa/uthibisho umetolewa mbele yangu leo hii, tarehe.....Mwezi.....Mwaka.....

**KAMISHNA WA VIAPO**

Au;

Mimi.....natamka kwamba nitakuwa mwaminifu na muadilifu katika kutekeleza majukumu yangu kama mdadisi katika sensa ya watu na makazi kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Takwimu, 2010, na sitatoa taarifa yoyote bila idhini kwa niaba hiyo au kuweka wazi au kutumia suala lolote au kitu ambacho kinanifikia kutokana na kuajiriwa kwangu kwa madhumuni hayo.

**MTOA TAMKO**

Tamko limetolewa mbele yangu tarehe .....Mwezi.....Mwaka.....

Jina .....

Wadhifa.....

Anuani.....

Sahihi.....



**JEDWALI LA TATU**

*(Limetengenezwa chini ya vifungu vya 22(1) na 24(1))*

1. Usajili wa Vifo, Vizazi na Matukio ya Jamii
2. Uhamiaji
3. Biashara ya Nje, Urari wa Biashara na Utalii
4. Taarifa za Kiuchumi
5. Kilimo
6. Ujenzi
7. Viwanda (Madini, Bidhaa za Viwandani, Umeme na Maji)
8. Soko la Ajira
9. Fedha za Serikali, Sera za Kifedha na Sekta ya Umma
10. Umaskini na mgawanyo wa mapato
11. Masuala ya Jamii, Elimu, shughuli za Kazi na Viwanda pamoja na Vyama vya Waajiri, Waajiri wa na Watu Wengine kwa Ujumla
12. Benki, Bima na Masuala ya Fedha kwa Ujumla
13. Biashara na Shughuli za Kitaalam
14. Biashara ya Usambazaji wa Ndani wa jumla na Rejareja
15. Elimu na Afya
16. Usafiri na Mawasiliano katika sekta zote za Usafiri wa Nchi Kavu, Maji na angani
17. Madhara, ajali, na fidia
18. Akiba ya bidhaa za viwandani
19. Bahati Nasibu, misaada ya kujitolea na makusanyo mengine na umma
20. Umiliki wa ardhi, makazi na matumizi ya ardhi
21. Mamlaka ya Serikali za Mitaa
22. Uhalifu na haki
23. Mazingira
24. Utafiti katika ngazi ya kaya Binafsi
25. Ujasiliamali
26. Habari, Mawasiliano na Teknojia

34

**Na.9**

*Muswada wa Sheria ya Takwimu*

**2015**

27. Jamii,Ustawi wa Jamii, na huduma Binafsi
28. Jinsia/Jinsi
29. Hali ya Hewa
30. Biashara
31. Bei
32. Nishati
33. Uwekezaji
34. Maji Safi naMaji Taka
35. Utafiti na Kuendeleza Ugunduzi
36. Vito vya Thamani
37. Utawala
38. Matangazo
39. Sehemu zinazotoa huduma za uzalishaji

Imepitishwa na Bunge tarehe 26 Machi, 2015.

THOMAS KASHILILAH  
Katibu wa Bunge